Sheria Ya Mungu

“Kanuni kuu za sheria ya Mungu zimeunganishwa katika Amri Kuimi na zilifuatishwa katika maisha ya Kristo. Nazo zinadhihirisha upendo na mapenzi ya Mungu, na makusudi yake kuhusu mwenendo wa binadamu na mahusiano nazo ni sharti kwa watu wote katika kila kizazi. Amri hizi ni msingi wa agano la Mungu na watu na kanuni katika hukumu ya Mungu. Kupitia utendaji wa Roho Mtakatifu zinadhihirisha dhambi na kuamsha haja ya kumpata Mwokozi. Wokovu ni kwa neema, na si kwa matendo, lakini matunda yake ni utii kwa Amri Kumi. Utii huu hukuza tabia ya Kikristo na huwa na matokeo ya ustawi. Ni ushuhuda wa upendo wetu kwa Bwana na wajibu wetu kwa wanadamu wenzetu. Utii wa imani hudhihirisha uwezo wa Kikristo katika kubadilisha maisha, na hivyo kuimarisha ushuhuda wa Kikristo. (Kut. 20:1-17; Zab. 40:7,8, Mat. 22:36-40, Kumb. 28:1-14; Mat. 5:17-20; Ebr.8:8-10; Yoh. 15:7-10; Efe. 2:8-10; 1Yoh.5:3; Rum. 8: 3, 4; Zab. 19:7-14).”

Macho yote yalielekea mlima. Kilele chake kilikuwa kimefunikwa na wingu zito lilioendelea kuwa jeusi hadi mlima wote ukazingirwa kwa usiri. Radi ilipiga kutoka gizani wakati ngurumo ziliposikika na kuakisiwa. “Mlima wa Sinai wote pia ukatoa moshi kwa sababu BWANA alishuka katika moto; na ule moshi wa tanuu, mlima wote ulitetemeka sana. Na hapo sauti ya baragumu ilipozidi kulia sana; Musa akanena, naye Mungu akamwitikia kwa sauti” (Kut. 19: 18, 19). Ufunuo wa Mungu ulitisha sana kiasi kwamba Waisraeli wote walitetemeka.” Mungu alipotoa amri zake Sinai, hakujidhihirisha tu kwamba ni Mtawala bali pia ni Mkombozi (Kut. 20:2). Ni Mwokozi ambaye hawaiti Israeli peke yake bali pia wanadamu wote (Mh. 12:13). Soma Kut. 20:1-17).

Asili ya Sheria ya Mungu
Sheria ya Mungu ni ya kimaadili, ya kiroho na yenye kubeba kanuni zinazojitosheleza.

Kuakisi tabia ya Mtoa Sheria
Kama alivyo Mungu, Sheria yake nayo ni kamilifu na ushuhuda wake ni safi (Zab.19:7, 8), Sheria ni takatifu, ya haki na njema (Rum. 7:12). Amri ni kweli na haki (Zab. 119: 151, 172).

Sheria ya Maadili
Sheria huonyesha mwenendo wa mfuasi wa Mungu anavyopaswa kuenenda. Kuacha kutii, huhesabika ni uasi. (1Yoh. 3:4)

Sheria ya kiroho
Sheria ni ya kiroho (Rum. 7:14). Kwa hiyo ni wale waliojawa Roho Mtakatifu ndio wanaoweza kuitii (Yoh. 15:4; Gal. 5:22, 23). Ni roho wa Mungu ndiye atuwezeshaye kuyafanya mapenzi yake (Mdo. 1:8, Zab. 51:10-12). Tunapokaa na Yesu, tunapewa uwezo wa kuzaa kwa utukufu wake (Yoh. 15:5). Sheria za kibinadamu huhusu matendo machache, bali sheria ya Mungu ni pana mno (Zab. 119:96). Katika hotuba ya Yesu ya Mlimani, Yesu alikazia hali ya kiroho ya Sheria ya Mungu kwamba dhambi huanza kwa kunuia kutoka moyoni (Mt. 5:21, 22, 27, 28; Mk. 7:21-23)

Sheria Chanya
Sheria inaposema usi inaamanisha unatakiwa kutenda jambo chanya. Kwa mfano, usiue (Kut. 20:13) ina sehemu chanya yenye kumaanisha kukuza/kulinda uhai.

Tunaitwa kuitazama sheria kwamba Mungu, kwa wema wake amefunua kanuni bora za haki zinazowazuilia watu wake mabaya yatokanayo na kumwasi.

Sheria Rahisi

Amri kumi kwa uzito wake ni rahisi. Ni fupi kiasi ambacho hata mtoto mdogo aweza kuzikariri na zinapenya kiasi kwamba hudhihirisha kila dhambi. Hakuna siri katika sheria ya Mungu. Wote wanaweza kweli ibebazo. “Mtu mwenye akili hafifu aweza kuzitambua kanuni zake na aliye mjinga aweza kuendesha maisha yake hata akafanyiza tabia inayofuatana na viwango vya kimbingu.”1SM p235.

Sheria ya Kanuni

Amri kumi ni muhtasari wa wa kanuni zote njema zinazotumika kwa wanadamu wote na kwa nyakati zote. Maandiko hutudai “mche Mungu na kuzitii amri zake, kwa kuwa hii ndiyo impasayo mtu (Mh. 12:13).

Maneno ya maagano (Kut.34:28) yamegawanywa kwenye sehemu mbili kama yalivyoandikwa kwenye mbao mbili za mawe (Kumb. 4:13). Amri nne za kwanza (Kut. 20:1-11), zinaelekeza wajibu wa mwanadamu kwa Mungu na sita za mwisho (Kut. 20:12-17) zinaelekeza wajibu wa mwanadamu kwa mwanadamu mwenzake. (Mt. 22:36-40; Luk. 10:27; Kumb. 6:4,5; Law. 19:18)

Amri ya kwanza yataka tumwabudu Mungu wa kweli peke yake, ya pili inazuia ibada ya sanamu, ya tatu inazuia watu kudhihaki jina la Mungu na ya nne inaita wanadamu kuikumbuka sabato ya Bwana na kumtambulisha Mungu kuwa muumba wa mbingu na nchi. Amri ya tano yawaita watoto kuwatii wazazi wao, (Kumb. 4:6-9; 6:1-7), ya sita hulinda maisha kwamba ni matakatifu, ya saba huingiza usafi na kulinda mahusiano ya ndoa, ya nane yalinda mali. Ya tisa hulinda ukweli na ya kumi inaenda kwenye mzizi wa mahusiano ya kibinadamu kwa kukemea kutamani ya mwanadamu mwingine.

Sheria ya Pekee

Amri kumi ni tofauti kwa kuwa zilisemwa na Mungu mwenyewe zikasikika na taifa lote (Kumb. 5:22) na pia ziliandikwa kwa chanda cha Mungu juu ya mbao mbili za mawe na kutunzwa kwenye sanduku la agano (Kut. 31:18; Kumb. 10:2).

Kuwasaidia Waisraeli kuzitumia sheria, Mungu aliwapa kanuni za ziada kuimarisha mahusiano yake na wao. Baadhi yake zinahusu mambo ya kijamii (Sheria ya kuongoza nchi), zingine zilihusu usimamizi wa ibada (Sheria za Kafara). Mungu aliwapa sheria hizi Waisraeli kwa kupitia Musa aliyeziandika kwenye kitabu cha sheria kilichowekwa kando ya sanduku la agano (Kumb. 31:25, 26) na siyo ndani ya Sanduku la Agano kama amri 10. Hizi sheria zilijulikana kama Kitabu cha Sheria cha Musa (Yosh. 8:31; Neh. 8:1, 2; 2Nyak. 25:4) au kwa urahisi, Sheria za Musa (2Waf. 23:25; 2Nya. 23:18).

Sheria ya Furaha

Sheria ya Mungu hutia moyo nguvu. Mtunga Zaburi alisema napenda sheria yako na ndiyo kutafakari kwangu mchana kutwa na pia sheria yako ni furaha yangu (Zab. 119: 97, 127, 143). Kwa wale wanaompenda Mungu, amri zake siyo nzito (1Yoh. 5:3). Kwa wenye dhambi, wanaona sheria inahuzunisha kwa kuwa nia ovu haiwezi kumtii Mungu (Rum. 8:7).

Makusudi ya Sheria
Mungu alitoa sheria yake kwa watu ili kuwajaza mibaraka tele na kuwaongoza wapate kuingia kwenye mahusiano naye yenye kuokoa. Madhumuni maalumu ya sheria ni: -

1. Hufunua mapenzi ya Mungu kwa Wanadamu
Kama maelezo ya tabia ya Mungu na mapenzi yake kwa wanadamu, sheria hudhihirisha nia yake na makusudi yake kwa wanadamu. Hudai utii mkamilifu, atakayetii yote akakosea juu ya moja, anakuwa amekosea juu ya yote (Yak. 2:10). Utii wa sheria kama kanuni ya maisha ni muhimu kwa wokovu wetu, Kristo mwenyewe alisema "kama ukitaka kuingia mbinguni, zishike amri" (Mt. 19:17). Utii unawezekana tu kwa uwezo wa Roho wa Mungu.

2. Ni msingi wa Agano la Mungu
Musa alipoandika Sheria na maelezo mengine, aliita Kitabu cha Agano (Kut. 20:1-24:8). Baadaye aliziita Amri Kumi Mbao za Agano (Kumb. 9:9 cf. 4:13)

3. Ni kipimo cha Hukumu
Kama ilivyo tabia yake, Sheria ya Mungu nayo ni haki (Zab. 119:172). Kila moja wetu atahukumiwa kwa sheria (Mh. 12:13, 14 cf. Yak. 2:12). Dhamiri za wanadamu hutofautiana. Zingine ni nyonge, na zingine zimenajisiwa, ovu au zimeunguzwa na pasi ya moto (1Kor. 7,12: Tit. 1:15; Ebr. 10:22; 1Tim. 4:2). Dhamiri zetu hutuambia tutende haki, lakini hazituambii haki yenyewe ni ipi. Hivyo sheria ndiyo kipimo cha hukumu.

4. Huonyesha Dhambi
Bila amri kumi, watu hawawezi kuuona utakatifu wa Mungu, hatia yao na hitaji la kutubu. Sheria ni kama kioo (Yak. 1:23-25) na wanaoitazama huona kasoro za tabia zao na kuona tunavyowajibika kwa Mungu (Rum. 3:19). Sheria hutufanya tuitambue dhambi (Rum. 3:20) kwa sababu dhambi ni uasi (1Yoh. 3:4). Kama sheria isingekuwapo, tusingejua dhambi (Rum. 7:7).

5. Hutuongoza kuongoka
Sheria ya Mungu ni zana cha Roho Mtakatifu kutuongoza kutubu. Sheria ya Mungu ni kamilifu, huuburudisha moyo (Zab. 19:7). Sheria ni kiongozi kutuleta kwa Kristo ili tuhesabiwe haki (Gal. 3:24). Kama kioo kisivyoweza kuondoa uchafu, sheria hutufanya tuhitaji chemchemi iliyofunguliwa (Zek. 13:1) na kusafishwa na damu ya Mwana Kondoo (Uf. 7:14).

6. Hutupatia Uhuru wa Kweli
Atendaye dhambi ni mtumwa wa dhambi (Yoh. 8:34). Nitakwenda panapo nafasi, kwa sababu nimejifunza kutii (Zab. 119:45). Yakobo aliita Sheria ya Mungu Sheria ya Kifalme, sheria ya Uhuru (Yak. 2:8; 1:25). Yesu anapotualika, hutuita kuchukua mzigo mwepesi na nira laini (Mt. 11:28, 29) na hiyo hutupa raha. Palipo na Roho wa Mungu, kuna uhuru (2Kor. 3:17).

7. Hukinga maovu na huleta Baraka
Kuongezeka makosa ya jinai, udhalimu, kukosekana uadilifu, na kuongezeka uovu ambako kumeijaa dunia kwa sasa kunatokana na kudharau Amri Kumi. Wakati sheria hii inapokubaliwa, hukinga dhambi, hukuza matendo mema na huwa njia ya kuimarisha haki.

Haki huinua taifa (Mith. 14:34; 16:12). Wale wanaokataa kutii amri za Mungu hawawezi kuikwepa laana (Mith. 3:33; cf. Law. 26; Kumb. 28). Kanuni hizi zina matokeo hata katika wakati wetu sasa.

Kudumu kwa Sheria

Kwa kuwa Amri Kumi, sheria ya maadili ni mwakisio wa tabia ya Mungu, kanuni zake siyo za muda mfupi au zinazohusiana na mazingira ila ziko kama zilivyo, zisizobadilika na zenye kusimama kwa wanadamu wote kwa nyakati zote.

Sheria kabla ya Sinai

Sheria imekuwapo kwa muda mrefu kabla ya kutolewa Amri Kumi kwa Wana wa Israeli. Kama sivyo, dhambi isingekuwapo kabla ya Sinai, kwa kuwa dhambi ni uasi (1Yoh.3:4).

Kwa kuwa Lusifa na malaika wake walitenda dhambi, hiyo hutupatia ushahidi wa kuwepo kwa sheria kabla ya uumbaji (1Pet. 2:4).

Adamu na Hawa walipoumbwa kwa sura ya Mungu, alifanyiza amri zake ndani ya mioyo yao na kwa kuasi kwao, dhambi iliingia kwa wanadamu (Rum. 5:12).

Baadaye, Mungu alimsema Ibrahimu kwamba alizitii amri zake na kuzitenda (Mw.26:5)

Musa alizifundisha Amri za Mungu kwa Waisraeli kabla ya kufika Sinai (Kut. 18:16)

Ukijifunza kitabu cha Mwanzo, utagundua kwamba amri za Mungu zilijulikana kabla ya kutolewa kwenye mlima Sinai.

Sheria kwenye Mlima Sinai

Wakiwa utumwani Misri, Waisraeli hawakumtambua Mungu wa kweli (Kut. 5:2) kwa kuwa waliishi katikati ya ibada ya sanamu na ufisadi. Kwa sababu hiyo walipoteza ufahamu wa utakatifu, usafi, na kanuni za kimaadili. Hadhi yao ya kuwa watumwa, iliwanyima nafasi ya kuabudu. Kuitikia kilio chao, Mungu alikumbuka agano lake na Ibrahimu na kuwaokoa kutoka kwenye tanuru la moto (Kumb.4:20) na kuwaleta kwenye nchi ambayo wangetii amri na sheria yake (Zab. 105:43-45). Mungu akatoa amri zake moja kwa moja kwa sababu ya uovu (Gal. 3:19) ili dhambi ionekane kwamba ni mbaya (Rum. 7:13).

Sheria ya Mungu kabla ya Kurudi kwa Yesu

Biblia huonyesha kwamba kabla ya Kristo kurejea, sheria ya Mungu itashambuliwa na Shetani na kufikia kilele chake. Atawaongoza watu wengi wasimtii Mungu (Uf. 12:9). Akitumia mamlaka ya mnyama, atautaka ulimwengu umwabudu mnyama badala ya Mungu (Uf. 13:3, 12).

1. Kushambuliwa sheria

Danieli sura ya 7 huonyesha mamlaka yenye kushambulia sheria ya Mungu kama Pembe Ndogo. Wasomaji wa Biblia wamezitambua falme za sura hii kuwa ni Babeli, Umedi/Uajemi, Ugiriki na Rumi. Pembe kumi ni falme kumi zilizotokea baada ya dola ya Rumi kuanguka mwaka 476BK. Maono ya Danieli yanasimama kwenye Pembe ndogo ambayo inatesa watakatifu, inanena kinyume chake aliye juu na kuazimu kubadili majira na sheria. (Dan. 7:25). Mamlaka hii itaendelea hadi Kristo atakaporejea. Maono yanakwisha kwa uthibitisho kwamba Mungu ataingilia kati na kuihukumu na kuingamiza Pembe Ndogo (Dan. 7:11, 26-28).

2. Watakatifu watailinda Sheria

Utii wa sheria utawatambulisha watakatifu kabla ya Kristo hajarejea mara ya pili. Wanazishika amri za Mungu na kuwa na ushuhuda wa Yesu (Uf. 12:17; Uf. 14:12). Katika kujiandaa kuja kwake Yesu, watahubiri injili wakiwaalika wengine kumwabudu BWANA kama mwumbaji. (Uf. 14:6, 7). Wale watakaomwabudu kwa upendo, hawataona amri za Mungu kuwa ni nzito (1Yoh. 5:3).

3. Hukumu za Mungu na Sheria

Hukumu ya Mungu ya mapigo saba ya mwisho kwa wasiotii inaanzia kwenye hekalu la hema ya ushuhuda mbinguni (Uf. 15:5). Israeli walilijua vema kwamba ni ile hema ambayo Musa aliifanya (Hes. 1:50, 53; 17:8; 18:2). Iliitwa hivyo kwa sababu ilibeba sanduku la ushuhuda (Kut. 26:34), ambalo lilikuwa na mbao za ushuhuda (Kut. 31:18). Kwa hiyo amri kumi ni ushuhuda kwa wanadamu juu ya mapenzi Mungu (Kut. 34:28, 29). Hata hivyo Ufunuo 15:5 inasema sanduku la ushuhuda lililoko mbinguni.

Hii ni kwa sababu Musa aliambiwa atengeneze nakala ya hekalu lililokuwa mbinguni (Ebr. 25:8, 40; cf. Ebr. 8:1-5). Amri Kumi halisi zimetunzwa pale. Kwamba hukumu ya mwisho itatokana na wanadamu kutomtii Mungu, kunafanya amri za Mungu kuwa za kuendelea daima. Kitabu cha ufunuo pia kinaonyesha kwamba hekalu la mbinguni lilifunguka na Sanduku la Agano likaonekana. (Uf. 11:19). Hekalu la duniani lilikuwa na sanduku la ushuhuda lenye amri za agano (Kut. 34:27; cf. Hes. 10:33; Kumb. 9:9). Hivyo ni dhahiri kwamba hukumu ya Mungu ya mwisho itahusu Sanduku la Agano lake lenye Amri zake asilia mbinguni (Uf. 11:18).

Sheria na Injili

Wokovu ni karama inayotufikia kwa neema kwa njia ya imani, siyo kwa matendo ya sheria (Efe. 2:8). Siyo tendo la sheria wala juhudi hata kama inasifiwa sana, wala siyo matendo mema, yawe mengi au machache, ya kujinyima au vinginevyo kwamba yaweza kumtakasa mwenye dhambi.(Tit. 3:5; Rum. 3:20). Maandiko matakatifu yanaelezea uhusiano wa sheria na injili, kila kimoja, kikishikilia kingine.

Sheria na Injili kabla ya Sinai

Adam na Hawa walipotenda dhambi, walijua nini ni hatia, hofu na hitaji. (Mwa. 3:10). Mungu aliwapa walichohitaji, kurejesha mahusiano yake na wao pasipo kutangua sheria yake. Injili ni kwamba mzao wa mwanamke ndiye atakayeleta ushindi dhidi ya dhambi (Mwa. 3:15). Kwa kuamini kwamba kifo cha mnyama kiliwaondolea dhambi, walikubali kafara ya Kristo atakayekuja kuwafia, na kwamba wokovu wao ni kwa neema peke yake. Injili ndilo agano alilofanya Mungu na aliowachagua (Mw. 12:1-3; 15:4, 5; 17:1-9). Mara nyingi iliambatana na sheria (Mw.18:18, 19; 26:4, 5). Amana ya agano ni Mwana wa Mungu aliyechinjwa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. (Uf. 13:8). Neema ya Mungu ilianza kutenda kazi mara dhambi ilipoingia. Mtunga Zaburi anasema, “Bali fadhili za BWANA zina wamchao, Tangu milele, hata milele--- Maana wale walishikao agano lake, na kuyakumbuka maagizo yake ili wayafanye (Zab. 103: 17,18).

Sheria na Injili Sinai

Utangulizi wa Sheria unamtambulisha Mungu akiwa mkombozi (Kut.20:1). Baada ya kuitoa Sheria, Mungu aliagiza Israeli wajenge madhabahu na kumtolea kafara ili wapatanishwe na

Mungu na kupokea mibaraka yake(Kut. 24:9 – 31:18). Wakati Amri Kumi ziliwekwa ndani ya Sanduku la Agano, kitabu cha sheria za maadhimisho kiliwekwa kando ya Sanduku kuwa ushuhuda (Kumb. 31:26).

Sheria na Injili Baada ya Msalaba

Kama wakristo wengi walivyoona, kifo cha Kristo kiliondosha sheria ya maadhimisho na kuimarisha sheria ya maadili. Ushahidi ni kama ifuatavyo: -

1. Sheria ya Maadhimisho

Kristo alipokufa, alitimiza alama za kuashiria kwa unabii juu ya mfumo wa kafara. Mfano ulikutana na kitu halisi. Kabla Yesu hajazaliwa, ilitabiriwa kwamba atakomesha mfumo wa kafara (Dan. 9:27). Siku aliyokufa, pazia la hekalu lilipraruliwa toka juu hadi chini kuonyesha kukoma umuhimu wa ibada za kafara za hekalu la duniani (Mt. 27:51). Ingawa Sheria ya Maadhimisho ilitimiza kusudi muhimu kabla ya Kristo, baada ya Yesu kufa msalabani, ilibakia kuwa kivuli cha mambo yajayo (Ebr. 10:1). Iliwekwa kwa kipindi kifupi hadi wakati wa matengenezo (Ebr. 9:10; Gal. 3:19) hadi Kristo alipokufa kama kafara halisi.

Kifo cha Yesu kilikomesha mamlaka ya mfumo wa kafara na kuugongomelea mslabani (Kol. 2:14, cf. Kumb. 31:26). Hivyo haikuwa muhimu kuendelea kutoa kafara zisizosafisha nia tena (Ebr. 10:4; 9:9; 14).

Hakuna haja tena ya Sheria ya Madhimisho ihusuyo vyakula, vinywaji, na maadhimisho ya Pasaka, Pentekoste, miezi mipya wala sabato za sikukuu. (Kol. 2:16; cf. Ebr. 9:10) ambavyo vilikuwa vivuli vya mambo yajayo (Kol. 2:17). Kama Wayahudi walivyotafsiri, Sheria ya Maadhimisho ilikuwa kikwazo, chenye kutenga Wamataifa hivyo Kifo cha Kristo kilivunja kiambaza na kuunda familia moja iliyoungana katika mwili moja kupitia msalaba (Efe. 2:14-16).

2. Amri Kumi na Msalaba

Kifo cha Yesu kilikomesha sheria ya maadhimisho na kuimarisha mamlaka ya Amri ya Maadili – Amri Kumi. Waumini wanakuwa watumishi wa haki na siyo watumwa wa dhambi (Rum. 6:14). Hivyo Wakristo hawatii Amri za Mungu ili waokolewe, badala yake wanatii amri kwa sababu wamekwisha kuokolewa. Hawaoni haja ya kutenda dhambi hata kama neema iliyowaokoa ni kubwa (Rum.6:1) Hakuna hukumu kwao kwa sababu wanatembea katika roho (Rum. 8:1).

Utii wa Sheria

Watu hawawezi kwa nguvu zao wenyewe kujipatia wokovu. Wokovu hupatikana kwa njia ya neema ya Mungu peke yake (Ef.2:8). Hata hivyo, utii wa sheria ni matunda kwamba tumeokolewa kwa neema (Tit. 2:11, 12).

Kristo na Sheria

Kristo aliziheshimu sana Amri Kumi. Ndiye aliyezitoa Sinai akiwa Mimi Niko (Yoh. 8:58; Kut.314) na utume wake ilikuwa kuitukuza Sheria (Isa.42:21). Maneno ya Zaburi yanaonyesha nia ya Yesu juu ya Sheria “Kuyafanya mapenzi yako Ee Mungu wangu ndiyo furaha yangu; Naam sheria yako imo moyoni mwangu (Zab. 40:8).

Aliianzisha imani iliyojali madai ya Amri za Mungu. Paul anauliza, je twaibatilisha torati kwa ajili ya hayo? Na anajibu la, badala yake tunaithibitisha (Rum. 3: 31). Yesu alimjibu kijana tajiri kwamba ikiwa anataka kuupata uzima wa milele, zishike amri (Mt. 19:17). Na ndiye aliyefundisha kwamba wasiofanya mapenzi ya Baba yake, hawataruhusiwa kuingia kwenye ufalme wa mbinguni (Mt. 7:21-24).

Yeye mwenyewe aliitii sheria na akaatuusia, amin nawaambia yodi moja wala nukta moja haitaondoka kwenye torati hata yote yatimie (Mt. 5:18). Akafundisha kwamba msingi wa Sheria ni upendo, kwa Mungu na kwa jirani (Mt. 22:36-40). Ndiye aliyesema anatoa amri mpya, ya kupendana (Yoh. 13:34) na akaagiza mpendane, kama mimi nilivyowapenda ninyi (Yoh. 15:12). Utii huonyesha upendo wetu kwa Mungu "Mkinipenda, mtazishika amri zangu" (Yoh. 14:15). Mkizishika amri zangu, mtakaa katika pendo langu (Yoh. 15:10). Vivyo hivyo, tukiwapenda watu wa Mungu, huwa tunampenda Mungu (1Yoh. 2:3). Hatutaweza lolote tusipokaa ndani yake (Yoh. 15:4, 5). Kwa kweli maisha yetu yatakuwa yamesulubiwa pamoja na Kristo (Gal. 2:20) na sheria yake itaandikwa mioyoni mwetu (Ebr. 8:10).

Baraka ya Kutii

Utii hukuza tabia ya kikristo na huleta afya, na kutufanya tukue hata tufanane na Kristo (1Pet. 2:2; 2Kor. 3:18). Mabadiliko haya, ni ushuhuda mwema kwa nguvu ya Kristo. Heri wanaomtii Mungu (Zab. 119:1), wanaotafakari sheria yake mchana na usiku (Zab. 1:2). Baraka za utii ni nyingi: -

(**1**)kupata hekima (Zab. 119:98, 99), (**2**) amani (Zab. 119:165; Isa. 48:18), (**3**) haki (Kumb. 6:25; Isa. 48:18) (**4**) moyo safi na adilifu (Mith. 7:1-5), (**5**) ufahamu wa ukweli (Yoh. 7:17), (**6**) kulindwa na maradhi (Kut. 15:26), (**7**)maisha marefu (Mith. 3: 1, 2; 4:10, 22) na (**8**) uhakika kwamba sala zitajibiwa (1Yoh. 3:22; Zab. 66:18).

Mungu anapotualika tumtii, ametupatia ahadi nyingi (Law. 26:3-10; Kumb. 28:1-12). Tunapomtii, tunakuwa tunu kwake na hutupa ukuhani wa kifalme (Kut.19:5, 6; cf. 1Pet. 2:5, 9) tukiinuliwa kuliko mataifa kwa kuwa ni kichwa na siyo mkia (Kumb. 28:1, 13).